Vilevile hakuna hali ya kutokuwa na uhakika kwa kiwango cha juu au harar kuhusiana na michango.

5. Vyombo vya uwekezaji

Waendeshaji wa Takaful huwekeza fedha kwa uwajibikaji wa hali ya juu katika kampuni ambazo zimedhihirisha viwango vya juu vya maadili na ambazo hazizababishi madhara kwa watu wa mazingira hasa, biashara zenyewe pamoja na bima zinafaa kujiepusha na uhusiano wa aina yoyote na shughuli za kamari, pombe, nyama ya nguruwe, silaha, tumbaku, na shughuli za kutoza riba, taaisi za ki fedha za kiislamu zimesambazwa huduma zao hadi kwenye masoko ya kifedha kwa kuanzisha sukuk (hati za thamani za Kiislamu) kama njia mojawapo ya uwekezaji na njia ya kukusanya rasilimali za kifedha.

Mpango wa Takaful una bima za aina gani?

Hakuna tofauti kubwa kati ya huduma za bima zinazotolewa na waendeshaji wa bima wa kawaida. Waendeshaji wa Takaful wanaendesha bima ya maisha na bima ya Jumia.

Bima ya jumia inaitwa Takaful ya Jumia na inahusisha kategoria kama vile bima ya magari ya kibiashara na kibnafsi, ajali ya mtu Binafsi, Bima ya ubaharia, moto wa Nyumbani, Moto wa Viwandani, matibabu n.k.

Bima ya maisha inajulikana kama Takaful ya Jamaa na inajumuisha maisha kwa jumia, Malipo yanayostahili,malipo ya kila aina ya sere za kiuwekezaji miongoni mwa mengine.

Aidha, bima kwa wenye bima chini ya mfumo wa takaful inaitwa Re-Takaful.

Ni nani anayeweza kukata bima ya Takaful?

Mtu yeyote anaweza kukata bima ya Takaful. Takaful si kwa Waislamu tu. Kwa kuwa inategemea sana kaida ya ushirikiano, ina manufaa sawa kwa wanajamii wote bila ubaguzi wowote na kwa hivyo basi iko wazi kwa kila mtu.

Insurance Regulatory Authority
Bima Bora kwa Taifa
IRA

Insurance Regulatory Authority
Zep-Re Place, 7th Floor
Upper Hill, Longonot Road, off Kilimanjaro Avenue

P.O. Box 43505 GPO 00100, Nairobi Kenya
Tel: +254-20-4996000
Mobile: +254 - 719 047000
Email:commins@ira.go.ke

Help Desk
Toll-free Line: +254 - 0800724499
Email: customercare@ira.go.ke
complaints@ira.go.ke
ethics@ira.go.ke

Insurance Fraud Investigation Unit
Hotline: +254 - 707598455, +254 - 786595455
Email: ifiu@ira.go.ke

Policyholders Compensation Fund
Tel: +254-20-4996238
Email: info@pcf.co.ke

IRAKenyaPage @ira_kenya

www.ira.go.ke

Insurance Regulatory Authority
Bima Bora kwa Taifa
IRA

MWONGOZO WA TAKAFUL

www.ira.go.ke

MWONGOZO WA TAKAFUL

Takaful ni nini?

Takaful ni aina ya bima ya kislamu iliyo na misingi kwenye Shariah.Imebahinishwa ya kuwa bima ya kawaida haiandamani na mahitaji ya Shariah. Kutengana na Shariah kunatokana hasa na mkataba wa bima na biashara ya bima kwa jumla. Masuala yanayofungamana na mikataba ya bima ni pamoja na riba, gharar, na maysir.

Huku tofauti zinazotokana na uendeshaji wa shughuli za soko la bima zikiwa zinaweza kushughulikiwa na waendeshaji wa Takaful kubuni upya taratibu za uendeshaji na uhasibu ili kuzifnya kuambatana na shariah, zile zinazohusiana na mikataba ya bima zinahitaji ukarabati wa mikataba ya bima yenyewe.

Historia ya Takaful

Takaful,kama dhana mbadala ya bima illibuka kule sudan, barani Afrika mnamo mwaka wa 1979 na kufika sasa imeasambaa hadi mashariki ya kati, uropa na marekani na maeneo mengine ikiwemo Kenya na ulimwengu kwa jumla. Mashirika makubwa ya kimataifa kama vile chartis, hannover, HSBC miongoni mwa mengine yamekubali mfumo wa takful kama njia mojawapo ya kuendesha biashara ya bima.

Takaful huendeshwaje?

Kanuni za Takaful zina misingi yake kwenye ushirikiano, uwajibikaji, uhakikisho, ulinzi na usaidizi miongoni mwa makundi ya washiriki. Ni aina mojawapo ya bima ya pamoja. Msingi wa Takaful si kwa minajili ya kupata faida bali ni kushikilia ile kanuni ya kusaidiana kubeba mizigo yetu" Takaful ni njia ya kuzia hasara kupitia hazina iliyoundwa na washiriki wanaokubali kusaidiana wakati wa haja.

Takaful inategemea michango kutoka kwa washiriki (tabaru) badala ya ada za kawaida zinzotozwa na kampuni za kawaidi za bima. Kampuni za bima za takaful huweka mipaka bayana kati ya washiriki na waendashaji. Wajibu wao hauna mamlaka yanayozidi usimamizi wa bima na kuwekeza

michango ya washiriki kwa niaba yao katika vyombo vya kifedha ambavyo vinaadamana na matakwa ya shariah. Takaful ina kanuni tano za kimkataba ambazo zinaipata umahususi miongoni mwa bima za kawaida.

Kanuni hizi ni:

1. Mkataba wa bima ya pamoja kati ya washiriki wenyewe

Takaful inamhitaji kila mshiriki kutoa mchango au tabaru kama tu ilivyo katika bima za kawaida, kiasi cha mchango wa kila mara kinachotolewa na kila mshiriki ni tofauti na cha mwenzake kutegemea kiasi cha hatari katika bima za jumla (Takaful ya jumla) na kiwango cha pesa kilichokatiwa bima katika bima ya maisha (Takaful ya jamaa).

2. Msaada ikiwa hasara itatokea

Msaada wa kifedha hutolewa kwa mshiriki ambaye atapatwa na hasara au uharibifu. Malipo haya yanatokana na michango inayotolewa na kila mshiriki.

3. Kuzichukua pamoja hasara za ziada

Baada ya malipo ya fidia ya takaful kukamilika, fedha za ziada zinazobakia zinalipwa wa shiriki ambaopia wanawajibika kulipia nakisi zozote zinazotokana na uendeshaji wa hazina hii mwendeshaji wa Takaful (wasimamizi) analipwa kwa kazi ya usimazi anayoitekeleza.

4. Kuondoa kamari na kutokuwa na uhakika

Hivi, hakuna kamari au kujilimbikizia mali kwa njia haramu katika mpango wa Takaful, kwa kuwa hazina hii ni mali ya washiriki, zoezi hili halinuii kuzoa faida kwa kuwalaghai wenzako.